

LbE 2012 “Everyone’s different – Respect for Minorities

Episode 06

A Hostile New Home – Xenophobia in South Africa

Author: Leonie March

Editor: Katrin Ogunsade

Proofreader: Charlotte Collins

Characters

<i>Narrator</i>	female	about 30	english
<i>Marie</i> <i>(pseudonym)</i>	female	in her mid 30s	english
<i>Baruti Amisi</i>	male	in his mid 40s	english
<i>Jahmil Qubeka</i>	male	in his early 30s	english
<i>Collage of 3</i> <i>South Africans</i>	2 female voices 1 male voice		english

Intro:

Karibu katika sehemu ya sita ya kipindi chetu cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako** kuhusu kuzingatia haki za jamii za watu walio wachache barani Afrika. Leo tunashughulikia suala nyeti la chuki dhidi ya wageni nchini Afrika Kusini. Chuki hiyo inatokana na hofu isiyo na msingi kwa wageni. Hali hii haipo Afrika Kusini pekee bali hupatikana kila mahali ulimwenguni. Miaka michache iliyopita visa vya kuvamiwa raia wa kigeni viliongezeka kwa kasi nchini Afrika Kusini. Leo hii, wahamiaji hasa kutoka mataifa mengine ya Afrika wanaishi maisha ya hatari nchini Afrika Kusini. Hata hivyo, serikali ina mikakati thabiti kuzuia wageni kushambuliwa. Mikakati hiyo inaelekea kusaidia kudhibiti mambo.

1. Sound: Durban Downtown

2. Narrator:

Eneo la madukani la jiji la Durban lina shughuli nyingi. Madereva wa magari wanapiga honi ovyo ovyo wakitafuta wateja, kuna makundi ya watu wanaovuka barabara, kandoni mwa barabara kuna vibanda vidogo vya wanawake wanaochuuza bidhaa mbalimbali. Kwangu mimi Marie ni sawa na raia wengine wala sioni tofauti yoyote. Amembeba mwanae kwenye kigari anachokisukuma. Amevaa shati la rangi ya waridi na sketi ndefu nyeupe. Marie ana umri wa miaka thelathini na sita na ni mkimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ananiambia kwamba wenyeji wanamuona daima kuwa mgeni, na kwamba hatakiwi kuwepo Afrika Kusini.

3. Marie:

Mungu tu ndiye anayetuhifadhi hapa Afrika Kusini. Tunajua vizuri kwamba hawa watu hawatupendi hata kidogo. Kila mara husema: “Nyinyi Makwerekwere!” Shida kubwa mtu kwenda sokoni kama hujui lugha. Wanazungumza lugha yao. Usipoelewa wanasema “Hamba, Makwerekwere!” Kisha wanakufukuza.

4. Narrator:

“Makwerekwere” ni neno la matusi linalotumiwa Afrika Kusini kuwaita wahamiaji hasa kutoka mataifa ya Afrika. Neno hilo lilianza tangu mwaka 2008, wakati mashambulio ya chuki yalipoanza kwenye makazi ya watu weusi- maeneo ambayo raia weusi walilazimishwa kuishi katika enzi ya ubaguzi wa rangi. Wahamiaji wengi walipigwa na kuteketezwa kwa moto nchini humo. Wengine walijeruhiwa; maduka yao yakaporwa na nyumba zaio zikaharibiwa.

KW begin

Marie aliyekimbia vita nchini mwake, mpaka sasa anaogopa kutumia jina lake halisi. Anakumbuka wakati huo wa mauaji ya wahamiaji.

5. Marie:

Wanasema: “Wewe ni mgeni, unafanya nini nchini mwetu? Rudi nchini kwako.” Wanaweza kukupiga. Wanaweza kukutenda lolote. Wakati huo tulilazimika kukimbilia kanisani na kulala humo humo. Tulikaa kanisani kwa muda wa miezi miwili hadi mitatu bila kutoka nje. Mchungaji alituletea chakula humo. Watoto wetu hawakuhudhuria shule kwa muda wote huo wa miezi mitatu. Hali ilikuwa mbaya.

KW end

6. Narrator:

Hali ilikuwa mbaya zaidi hasa mwaka 2008; lakini chuki kwa wageni lilikuwa jambo la kawaida, na mpaka sasa kuna chuki katika maeneo ya watu maskini na pia mijini. Baruti Amisi anayajua haya kwa uhakika. Na yeye pia ni mkimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Sasa hivi ni mtafiti katika Chuo Kikuu cha Kwazulu Natal.

7. Baruti Amisi:

Niliwasili Afrika Kusini mwaka 1997. Tumeshuhudia visa vingi vya chuki kwa wageni: niliwahi kushuhudia watu wakipigwa visu kwa kushindwa kuzungumza baadhi ya lugha za kienyeji, na nimeshuhudia watu wakiuwawa kwa sababu hiyo. Katika eneo la Magharibi jijini Cape Town watu huuwawa na miili yao ikakatwakatwa vipande vipande. Maanake chuki inaweza kusababisha binadamu kutendea binadamu wenzao unyama. Wanauwa watu na kukatakata miili yao vipande vipande. Hayo yalitukia kabla ya mwaka 2008.

8. Narrator:

Si raia wote wa Afrika Kusini wanaowachukia raia wa kigeni. Wengi waliwasaidia sana wakati mashambulio yalipokuwa yamezidi. Wengine, mathalani, mtayarishaji filamu Jahmil Qubeka, walianza kupinga hadharani chuki kwa wageni mwaka 2008.

9. Jahmil Qubeka:

Nilitahayari sana wala sikuonea fahari uraia wangu wa Afrika Kusini. Hisia za masikitiko zilitawala moyo wangu: "Mungu wangu, mbona haya

yanatukia nchini mwetu?” Ni jambo la kusikitisha kweli. Sisi raia wa Afrika Kusini, tulikuwa wakimbizi katika mataifa mengine wakati wa siasa za ubaguzi wa rangi. Sasa hatutaki kuwavumilia watu wengine. Hilo jambo liliniumiza moyo kupita maelezo.

10. Sound: Township

11. Narrator:

Hali katika makazi ya weusi mijini ingali tete. Wahamiaji na wakimbizi wa Kiafrika wanaokuja Afrika Kusini wakitaraji maisha mema wangali wakishambuliwa. Ghasia sampuli hiyo husababishwa na upungufu wa ajirana makazi kwenye maeneo ya watu maskini. Raia hawa watatu wa Afrika Kusini wanaelezea hisia za wenzao wengi.

12. Collage:

Hawa wageni ni kikwazo kikubwa kwetu sisi. Hawaimarishi uchumi wa Afrika kusini. Faida wanazopata wanazipeleka makwao.

(woman)

Watu wana hasira. Wako tayari hata kuuua ili wapate nyumba za makazi.

(young man)

Hatuwataki hapa. Afrika Kusini ni taifa la raia wa Afrika Kusini pekee. Tuliipigania nchi ya Afrika Kusini. Nchi hii sasa ni yetu. Uhuru ni wetu.

(woman)

13. Narrator:

Uhuru huo ndio unaowavutia Waafrika wengine kutoka mataifa masikini yaliyo na mizozo. Wahamiaji halali na wasiokuwa halali nchini Afrika Kusini, wanakisiwa kuwa kati ya milioni tatu na milioni saba. Maelfu ya watu waliokimbia mashambulio ya mwaka 2008, wangali wakiishi makanisani na maeneo mengine. Wanaogopa kurejea kwenye makazi ya watu weusi.

14. Sound: Apartment, distant traffic and voices

15. Narrator:

Marie, mumewe na watoto wao watano wanaishi katika nyumba iliyopo kwenye jengo lililo katikati ya jiji la Durban. Nyumba yenyewe haitoshi: chumba kimoja cha kulala na chumba kidogo cha maongezi, ambacho nyakati za usiku huwa chumba cha kulala watoto. Sehemu kubwa ya kipato chao huishia kwenye kodi. Hata hivyo, wanajihisi salama kwa kiasi fulani.

16. Marie:

Sehemu za makazi za watu weusi ni hatari sana. Tunaogopa kuishi huko kwa sababu ya uhalifu. Wanaweza kukuuwa. Kuna mtu atakutafuta kweli? Hakuna. Wanaweza kuiba kila kitu ulicho nacho. Ndiyo sababu raia wengi wa kigeni wanaishi mijini. Maisha ni magumu, kwa sababu yetu sisi kuishi hapa: Kodi juu, umeme, maji. Kwenye makazi hayo ya weusi gharama si kubwa. Lakini hatuwezi kuishi huko.

17. Sound: Durban street & voices

18. Narrator:

Lakini hata hapa mjini, chuki kwa wageni ni jambo la kila siku. Wahamiaji kutoka mataifa mengine ya Afrika si sana kuwapata wakishambuliwa, lakini wanatukanwa, kubaguliwa na kubahudhiwa.

KW begin

Marie na familia yake wamewahi kuyapitia hayo. Watoto wake hutukanwa shuleni. Mwenye nyumba yao ya zamani aliwafukuza kutoka nyumba yake kwa kisingizio cha kutaka kuikarabati.

KW end

Mtafiti Baruti Amisi, ambaye pia ni Ofisa Mkuu Mtendaji wa Baraza la Wakimbizi la Halmashauri ya Kwazulu Natal, amewahi kupokea visa vingi mfano wa hicho cha Marie.

19. Baruti Amisi:

Baadhi ya wenye nyumba wako radhi kuwapa nyumba zao raia wa kigeni. Kwa nini? Hawatalalamika iwapo nyumba hazitakarabatiwa mara kwa mara, ni rahisi kuwatatiza, hawajui haki zao. Ni rahisi kuwabahudhi kwa kuwa hawana watetezi. Hata nikawapigia simu polisi sasa hivi, watakuja kesho kwani lafudhi yangu wanaisikia. Watoto wetu hawapewi nafasi katika shule ati kwa visingizio kwamba hatuwezi kulipa karo. Kina mama wajawazito ambao ni wamkimbizi hutatizika sana wanapokwenda kujifungua, kwa kuwa si raia wa Afrika Kusini. Kuna chuki za aina nyingi. Huwezi kuamini. .

KW begin

20. Sound: Church, singing / Or repeat Sound 14 apartment

21. Narrator:

Marie amempakata bintiye wa umri wa miezi tisa. Anasema kwamba hata makanisani raia wa kigeni pia wanachukiwa. Marie ni mkiristo na Wakongo wengine wenzake yeye ni mfuasi wa madhehebu ya kiinjilisti, jijini Durban. Kanisa lao linawahudumia wakimbizi. Anasema alishtuka alipomsikia mchungaji, raia wa Afrika Kusini akiunga mkono chuki kwa wageni.

22. Marie:

Ajabu – yeye ni mchungaji, alijua kweli tupo, lakini akasema: Tumechoshwa na hawa wageni. Ni lazima warudi majumbani mwao. Wanatupokonya kazi zetu, wanawaoa mabinti zetu. Anayasema haya hadharini, tena ni askofu mwenye kanisa kubwa, anawashauri jinsi ya kukabiliana na raia wa kigeni. Ndiyo sababu tunasema: Hawa watu hawawezi katu kutupenda.

23. Narrator:

Marie anatikisa kichwa chake kwa masikitiko. Haelewi kwa nini watu wengi nchini hapa wanawachukia Waafrika wenzao. Watafiti pia wanalishughulikia suala hili.

KW end

Baruti Amisi amechunguza sababu za kuwepo chuki dhidi ya wageni na amepita hoja kadhaa. Ukosefu mkubwa wa kazi; raia wengi wa Afrika Kusini wanawashutumu wageni kwa kuwakosesha nafasi za kazi kwani wao wako tayari kulipwa mishahara duni. Kuna ushindani kwenye

maduka ya rejareja; mara nyingi raia wa kigeni wanaofanya biashara ya maduka ndio wanaoshambuliwa. Katika maeneo ya maskini kuna matatizo ya makazi. Jambo hili pia linachangia chuki kuwepo. Raia wengi wa Afrika Kusini hawatofautishi baina ya wakimbizi na wahamiaji wanaokuja kwa sababu za kiuchumi.

24. Baruti Amisi:

Usipotafoutisha baina ya wanaokuja kutafuta ajira na wale waliokimbia kunusuru maisha yao, raia wa kawaida wanachukulia kuwa kila wanayemuona amekuja kuwapokonya kazi zao. Kwa hivyo, wengine wanakisia kuwa, hawa watu wamekuja kuwatorosha wanawake wetu, wanakuja kwetu kutupokonya kazi zetu, wanakuja hapa kutuletea maradhi na uhalifu.

KW begin

Basi kutegemea mtazamo huo wa hofu na kuvamiwa, bila shaka watakuwa mbioni kujihami. Kwa hivyo, wanashambulia mahasimu wao kabla ya wao kushambuliwa, kwa kuwa hao wageni ni wahalifu, wanauza dawa za kulevya, wanaleta maradhi, wanawatorosha wanawake wao na kuwapokonya kazi.

KW end

25. Sound: Refugee council, distant voices

26. Narrator:

Baruti Amisi yumo katika ofisi yake ndogo ya Baraza la Wakimbizi la Kwazulu Natal katikati ya Jiji la Durban. Baraza hilo linajumuisha jamii takriban ishirini zinazoshughulikia wakimbizi mkoani humo pamoja na mashirika mengine. Ziada ya huduma za kila siku kwa wakimbizi, kina Baruti mara kwa mara, hutayarisha makongamano katia maeneo maskini zaidi katika jiji hilo.

27. Baruti Amisi:

Tunaandaa makongamano yanayowajumuisha raia wa Afrika Kusini na wageni kujadili maswala yanayowaathiri. Katika harakati hizo watu hugundua kuwa shida ni za kila mmoja wao. Kwa hivyo, badala ya kupigana wanapaswa kuungana.

28. Narrator:

Baruti Amisi anasema mkakati huo wa kushughulikia matatizo ya makundi hayo mawili kwa pamoja, unasaidia sana.

29. Baruti Amisi:

Tunaweza kuzuia mashambulio yanayochochewa na chuki katika maeneo ya makazi ya raia weusi wa Afrika Kusini. Kwanza: watu wanajadiliana. Pili: kupitia mitandao tulio nayo, watu wanaweza kueleza maeneo yanayozusha mihemko, mambo yanayoweza kusababisha mihemko na mahali ambapo hali inaweza kudhibitiwa kabla ya kuzuka ugomvi. Kwa hivyo, kazi yetu inasaidia kwa kiasi kikubwa.

KW begin

Kusema kweli, ni dalili nzuri inayoashiria kufanikiwa kwa azma yetu pale watu wanapoanza kuzungumzia na kuridhia ushirikiano, udugu na umoja katika jamii.

KW end

30. Narrator:

Baruti Amisi anatumai kwamba miradi mingine kama huo wake, itafadhiliwa siku za usoni, ili hizo chuki zishughulikiwe mapema bila kusubiri mauaji ya wahamiaji. Kinga ni bora kuliko tiba.

Outro:

Tunatumai umefurahia kusikiliza kipindi chetu cha leo cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako** kuhusu **kubaguliwa wahamiaji nchini Afrika Kusini**. Mwanahabari wetu alikuwa Leonie March. Ukitaka taarifa ya ziada, kusikiliza tena sehemu hii, au vipindi vingine vya **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe. Tunakushukuru kwa kutusikiliza. Kumbuka kututegea sikio katika sehemu inayofuata. Kwaheri.